



Fifth EsF Assembly
Hyderabad, India
30 July-August 13, 2016

Montessori Education for Social Change
Serving Humanity - Celebrating Solidarity

2016 EsF Assembly Daily Summary

Tuesday, 2 August 2016

Yoga na matembezi ya asili yaliendelea asubuhi na mapema kwa washiriki wa WwM. Kazi ya siku ilianza rasmi saa 9 asubuhi kwa Lynne Lawrence kwa kunukuu Margaret Mead na kugawana lulu toka siku iliyopita. Phillip O'Brien aliwasilisha mada juu ya Umoja wa Mataifa ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (MME). Philip aliwasilisha taarifa ikijumuisha toka kucheza hadi majadiliano. Alielezea jinsi Malengo ya Maendeleo Endelevu yalivyochipuka toka Malengo Endelevu ya Milenia. Katika MME neno 'endelevu' limekuwa na umuhimu mkubwa. Phillip pia alitujulisha juu ya uchapishaji utakaotolewa na Shirika la Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo (SUKM) lijulikanalo kama 'Mwelekeo Kujenga Elimu 2016'. Maswali juu ya SUKM yalikuwa juu ya maisha ya baadaye ya familia, mustakabali wa taifa – nchi, na kama miji ndio nchi nyingine. Majadiliano yaliendelea kuhusu ujasiri wa ulimwengu mpya. Lynne alitrudisha kwenye majadiliano kuhusu Malengo ya Maendeleo Endelevu na kusema kwamba ni muhimu kwa Montessori kufanya kazi zake kwa mwelekeo huo. Aliwapa changamoto washiriki kuja na kauli ya kuunganisha siku ya mwisho wa mkutano.

Wakati wa chakula cha mchana. Video juu ya Mtoto katika asili ilionyeshwa kwa washiriki waliohitaji. baada ya chakula cha mchana kulikuwa na wasilishaji wa mada mbili zilizotolewa na wanamontessori ambao walihifadhi safari ya shule zao. Parimala Rani Thipparthy aliorodhesha changamoto katika kuendeleza shule za vijijini na katika kijiji cha Gopalpet katika mji wa Telangana. Monica Ferri alizungumzia juu ya uwazishwaji wa Fundación Dejemos Huellas ili kuwasaidia watoto wenye kipato cha chini na maendeleo ya Escuela Monte Carmelo iliyopo Ecuador.

Washiriki walijiunga kwenye makundi yao ya kazi ili kuzungumzia maadili na kanuni muhimu, maanadalizi ya waelimishaji na kupata hadithi. Mkutano ulikaa pamoja kwajili ya majadiliano na maswali mwishoni. Kazi nyingine za siku zilikuwa ni zaununuzi wa nguo za kihindi, lulu na mapambo, ununuzi wa vitabu vya Kimontessori na kupaka hina.
